4th COMMUNITY OF PRACTICE FOR LEARNER-CENTRED EDUCATION

JUHUDI ZA KUONDOA WINGU ZITOLILILOPOKATI YA MUHTASARI YA MASOMO NA UTENDAJI KWA WALIMU

(*MWL. EMMANUEL M. ENOCK-MWADUI S/M, SHINYANGA MANISPAA*)

LILILOPOKATI YA MUHTASARI YA MASOMO NA UTENDAJI KWA WALIMU

Muhutasari wa masomo ni mwongozo maalumu ulioandaliwa kitaalamu kumsaidia mwalimu afundishe kwa kuzingatia malengo ya elimu yanayokidhi viwango vilivyowekwa na taasisi ya ukuzaji mitaala. Muhtasari ni lazima uandaliwe kwa kuzingatia masuala ya kitaaluma, kijamii na tekinolojia kadri yanavyojiri. Wizara kupitia kitengo chake cha ukuzaji mitaala imewapatia dhamana walimu wachache kufanya kazi hiyo nyeti ya kuandaa mitaala iishirikiana na taasisi mbalimbali za kielimu ili kuhakikisha elimu yetu haipitwi nawakati hli ni jambo jema kwani upo usemi usemao “panya wengi hachimbi shimo” kwa maana hiyo walimu wote tusingeweza. Naipongeza serikali kuwa makini na mabadiliko na kutoa miongozo inayoenda na wakati

Mabadiliko huwafikia walimu kwa kuanza aidha tetesi au kupitia vyombo vya habari kabla hata mihutasari husika haijawafikia. Nijambo la ajabu iliyo yakini kuwa mihutasari yenye mabadiliko huwafikia walimu wa darasani bila maolekezo ya kina wala uchambuzi ili kubaini kwanini kitu Fulani kimebadilika na kingine kimebaki kama kilivyokuwa. Mambo haya yote huweza kupatiwa ufumbuzi kwa kuzi ngatia mazingira halisi ya utendaji wa mwalimu. Mara nyingi utaona muhtasari umesema angalia kiongozi cha mwalimu! Suala hili limepelekea walimu walio wengi kufundisha mawazo yao wala si matakwa ya mtaala. Mfano, somo la Kiswahili kwa shule za msingi limekuwa likizua mitafaruku kuanzia kwa walimu, maafisa wa elimu hadi wakaguzi wa shule kitu ambacho ni hatari sana kwa taifa la Tanzania ambalo ndo chimbuko kuu la Kiswahili duniani. Je, kwa mtindo huu tutafika?

Hapa tulipo hakuna mgeni wa mabadiliko ya mtaala, tumewahi kushuhudia gharama kubwa ikitumika kuwaweka watumishi wa ngazi za juu wizarani, maafisa elimu wa mikoa na wilaya, wakaguzi wakuu wa shule wa kanda kuwapatia mafunzo juu ya mabadiliko ya mtaala tena siku zisizopungua 5 hadi 7. inapofikia ngazi ya watendaji wakuu, yaani walimu wa darasani utasikia hakuna fedha na kama itapatikana utaambiwa walimu watafanya mafunzo siku2 hadi 3. Na hao siyo walimu wote ni wateule wachache tu! Nasikitika zipo sehemu hadi leo niongeapo hawajaupata mhamo wa ruwaza kwa vitendo wanaimba wimbo tu lakini kiutendaji bado wamo mlemle tulimoambiwa kuhama!

UCHAMBUZI WA MUHTASARI

Uchambuzi wa mhutasari ni suala nyeti sana kwa walimu kulifahamu, hebu waulize walimu wangapi wamewahi kufanya uchambuzi wa muhtasari kwa kina kutegemeana na mazingira yao ya utendaji? Yawezekana ukapata jibu kuwa kila mtu anafanya kivyake tena ni ile kulenga mada zote ziingie katika mihula bila kujali kama zinawezekana ama la! Lengo la kufanya uchambuzi wa mhutari ni kuhakikisha kuwa mwanafunzi anajifunza kwa kuzingatia nyanja kuu za ujifunzaji yaani, Utambuzi, Mwelekeo na Vitendo. Hapa ndo tunapata hata aina gaini ya maswali na vitendo vya ufundishaji na ujifunzaji vinampatia mwanafunzi ujenzi wa maana ili awe na mwelekeo sahihi katika ujifunzaji wake. Wilaya ya Shinyanga yenye Halimashauri za Shinyanga na Manispaa kwa kushirikiana na shirika la OXFAM GB wamewezesha walimu kumudu uchambuzi wa mhutasari kupitia mradi wa EQUIP.

Zifuatayo ni nyanja na ngazi zake apaswazo mwalimu kuzijua na kuzizingatia wakati wa uchambuzi wa muhtasari.

UTAMBUZI

f) Tathmini

e) Uundaji

d) Uchambuzi

c) Matumizi

b) Ufahamu

a) Maarifa

MWELEKEO

e) Kuonesha mtindo

d) Kuwianisha masuala

c) Kuthamini

b) Kuitikia

a) Kuwa tayari kupokea

VITENDO

g) Ujuzi wa vitendo vya ubunifu

f) Ujuzi wa vitendo vya kukabili mazingira

e) Kufanya vitendo tata

d) Kutenda ipasavyo

c) Ujuzi wa kutenda

b) Ujuzi wa kuiga

a) kuhusisha vitendo

Uchambuzi wa muhtasari unapofanyika vizuri humwezesha mwalimu kufanya tathimini na upimaji wa mambo yote aliyojifunza mwanafunzi. Katika upimaji mwalimu ataweza kuandaa vyema jedwali la utahini. Ufuatao ni mfano wa mabo mazuri yaliyomo katika mwongozo wa upimaji na tathimini ambayo yalisitahili kuwafikia walimu;

Mfano wa jedwali la utahini lililo tumika katika somo la hisabati darasa la sita nyanja ya Utambuzi.

	Ngazi za kupimwa							
Mada zinazopimwa	Kumbukumbu	Ufahamu	Matumizi	Uundaji	Uchambuzi	Tathimini	Jumla ya maswali	% kwa staidi zote
1. Namba nzima	1		1			1	3	12
2. Muda		1	2				3	12
3.Sehemu	1			1			2	8
4. Desimali			1	1			2	8
5. Asilimia		2				1	3	12

6. Vipeo/ Vipeuo	1						1	4
7. Usafiri			1	1			2	8
8. Takwimu	1	1				1	3	12
9. Jometri			1	1	2		4	16
10. Alijebra	1	1					2	8
Idadi ya namba za maswali	5	5	6	4	2	3	25	100
% kwa kila ngazi	20%	20%	24%	16%	8%	12%	100%	

NB: *Jedwali kama hili na mengine mengi yawezayo kumsaidia mwalimu kuondoa wingu zito kati ya muhtasari na utendaji yamo ndani ya shelfu za Wizara na maafisa wa elimu badala ya shuleni ili mwalimu azione na kuzifanyia kazi*

NINI KIFANYIKE?

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi;

- Iandae mafunzo maalumu ya uchambuzi wa muhtasari ili kuwapata wawezeshaji mahiri walio walimu wa darasani ili wawe msaada kwa kila mkoa na wilaya kulingana na mazingira yao ya kiutendaji.
- Lianzishwe somo uchambuzi wa mhutasari ili wahitimu wa ualimu wawe wanamaliza wakiwa mahiri katika nyanja ya uchambuzi ili wasipate matatizo ya kiutendaji.
- Miongozo yote inayohusu mabadiliko ifike mapema shuleni ili kuondoa mashaka yasababishwayo na subira ya muda mrefu ipelekeayo walimu kukata tama.
- Kasima za MAFUNZO KAZINI.(dola 40 kwa kila mwalimu) zipelekwe moja kwa moja shuleni kulingana na idadi ya walimu kama ilivyo kwa fedha za capitation grants.
- Wizara itoe motisho kwa walimu wanaofanya vizuri ili kuamsha ari ya utendaji.

Maafisa Elimu Wilaya

- Wahakikishe wanafanya utetezi na ushawishi wa bajeti ya mafunzo kazini katika wilaya zao.

- Wawashirikishe waratibu elimu na walimu wakuu kupitia vikao vyao vya utendaji kila baada ya miezi mitatu.
- Washirikiane na Waratibu Elimu Kata kupata timu Mahiri za Wawezeshaji kwa ngazi za kata kwa kutumia walimu mabingwa wa masomo mbalimbali.
- Wajitahidi kupeleka nakala za moduli za uchambuzi wa muhtasari katika shule zote ili walimu wapate fursa ya kuzijadili na kuzifanyia kazi.
- Kupitia vikao vya utendaji wajadili na walimu wakuu na waratibu kuona hali ya utekelezaji wa muhtasari kwa mapendekezo ya ratiba yafuatayo; likizo fupi ya kwanza, likizo ya katikati ya mwaka, mara baada ya mtihani wa darasa la saba na mwishoni mwa mwaka.

Waratibu Elimu Kata;

- Wahakikishe uteuzi wa walimu mabigwa unafanyika kwa makini ili kuwapata walio mahiri katika taaluma na utaalamu katika ufundishaji.

- Wahakikishe kila shule inafanya uchambuzi wa muhutasari kwa kila somo kama sehemu ya maandalizi ya maazimio ya kazi.
- Wasimamie bajeti za mafunzo kazini zinazoandaliwa na wilaya na zile zinazoandaliwa na shule pia.
- Kila robo ya mwaka watoe taarifa ya utekelezaji wa muhtasari ili kuepuka jahazi la taaluma kwenda mrama.

Waratibu wa Vituo vya walimu

- Wakusanye maoni kuhusu maeneo tata katika mihtasari ya masomo na kuandaa warsha ili kuondosha ama kupunguza utata wa kiutendaji shuleni.

- Kwa kutegemea vyanzo vya mapato vilivyopo katika eneo la kituo, watenge fedha kwaajili ya ufanikishaji wa mafunzo kazini vituoni mwao.

- Waandae mpango kazi wa mafunzo kazini wa mwaka mzima katika vituo vyao wakishirikiana na walimu wakuu, waratibu elimu kata na maafisa elimu wa wilaya.

Walimu Wakuu na Walimu wa Taaluma shuleni;

- Wasimamie kikamilifu fedha za ruzuku za mafunzo kazini na washirikishe walimu katika kuandaa bajeti za mafunzo hayo.
- Wasimamie uchambuzi wa muhtasari shuleni kupitia waratibu wa masomo.
- Washirikiane na walimu kubaini maeneo yenye utata ta kuyatafutia ufumbuzi wa pamoja kulingana na mazingira ya yao ya kiutendaji.

Walimu wa masomo;

- **Washiriki kikamilifu kutoa hoja zinzobainisha mahitaji yao ya kiutendaji ili kutoa mwanga kwa waandaaji wa mafunzo kazini.**
- Washirikiane na walimu wenzao wa somo husika kwa madarasa yote ili kufanya uchambuzi wa muhutasari kwa lengo la kubaini viwango vya kufiri vinavyositahili kukuzwa kulingana na nyanja za ujifunzaji.

Rejea;

1. Taasisi ya Elimu Tanzania(2005) mwongozo wa mwezeshaji Elimu ya Msingi.
2. Taasisi ya Elimu Tanzania(2005) Mwongozo wa Upimaji na Tathmini kwa shule za Elimu ya Awali na Msingi.
3. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (2005), Muhtasari wa Kiswahili kwa Shule za Msingi Darasa la I-VII.